Jambo la kwanza kwa Mja.

أول واجب على العبد.

< سواحيلي – السواحلية – Swahili >

Shaykh Muhammad ibn Saalih al-'Uthaymeen
(Allah amrehemu)
سماحة الشيخ محمد بن صالح بن عثيمين (رحمه الله)

Imetafsiriwa na: Kitengo cha Lugha ya kiswahili, katika Tovuti ya IslamHouse.com
Imepitiwa na: Yunus Kanuni Ngenda.

ترجمة : فريق القسم السواحلي بموقع إسلام هاوس
مراجعة: يونس كنون نغندا

Jambo la kwanza kwa Mja.

Swali : Nilipi jambo la kwanza la wajibu kwa kiumbe?

Jawabu: Jambo la wajibu la kwanza kwa viumbe ni lile ambalo viumbe wanalinganiwa kwalo, na amelibainisha Mtume (s.a.w) kwa Muadhi bin Jabal (r.a) wakati alipomtuma kwenda Yemen, alimwambia: "Hakika unawaendea watu ambao ni mayahudi na manaswara, basi liwe jambo la kwanza utakalo walingania ni kutoa shahada ya Laa Ilaha ila Allah Muhamada rasulu Allah".

Imepokelewa na Imamu Bukhari (1496) na Imamu Muslim (19).

Hili ndilo jambo la kwanza ambalo ni wajibu kwa kila mja ashahidilie kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haqi ila ni Mwenyezi Mungu na Mtume (s.a.w) ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ni wajibu kwa waja wampwekeshe Mwenyezi Mungu, na waukubali na kukiri utume wa Muhamad (s.a.w), kwa kufanya hivyo ndio inapatikana Ikhlas na kufuata mambo hayo mawili ndio sharti ya kukubaliwa ibada.

Haya ndiyo mambo ya kwanza ambayo ni wajibu kwa kila mja kuyafanya, ampwekeshe Mwenyezi Mungu na akiri Utume wa Muhamad (s.a.w) na kutamka shahada ya (La ILLaha ila Allah Muhamada rasulu Allah) ndani yake ndiyo kunaTawhiidi yote.